**KISWAHILI**

**FASIHI (102/3)**

**KIDATO CHA TATU**

**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA TATU (OKTOBA 2023)**

# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

## SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI

1. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Mfalme ana watoto wawili wa kiume na anataka mmoja wao amrithi. Kwa sababu hataki kupendelea yeyote, anawapa changamoto ya kukimbia hadi mji wa mbali kwa farasi wao. Yule ambaye farasi wake atafika mwisho ndiye atakayemrithi. Ndugu hawa wanazembea jangwani kwa siku kadha kwa sababu kila mmoja anataka kufika wa mwisho. Hatimaye wanakutana na mzee mwenye busara ambaye anawapa wosia. Wanapanda farasi upesi na kutoka mbio ili wafike kwenye mji wa mbali walioagizwa na baba yao. Je, Mzee mwenye busara aliwaambia nini?

. i) Mafumbo

ii) Sifa zake

- ✓ Limefumba jibu
- ✓ -Linahitaji mtu kuwaza kwanza ili aweze kubaini fumbo
- ✓ -Limefumbia juu ya mambo yaliyomo katika jamii-farasi, wana, mfalme
- ✓ -Ni refu
- ✓ -Linahitaji mantiki ili kufumbua
- ✓ -Lina jibu lenye maneno mawili

(a) Wewe ni mmoja wa wanaowasilishiwa kipera hiki. Taja mambo matano utakayofanya ili ufanikishe uwasilishaji huu.
(al 5)

i. **Kushiriki kwa kupiga <u>makofi</u>**
ii. **Kuigiza baadhi ya <u>matukio</u>/matendo ya wahusika.**
iii. **Kuuliza <u>maswali</u>.**
iv. **<u>Hisia</u>/ishara wanazoonyesha usoni huweza kumfanya abadilishe uwasilishaji.**
v. **Kutoa – <u>majibu</u> kwa methali na vitendawili iwapo ngano itamalizikia kwa mtambaji kuwategea vitendawili.**
vi. **Kutoa mifano ya baadhi ya <u>wahusika</u> wa utugo kutoka jamii zao iwapo wataulizwa.**
vii. **Kutoa <u>funzo</u> katika utungo.**
viii. **<u>Kuitikia</u> - mh**
ix. **<u>Kucheka</u>/kulia.**
x. **<u>Kujibu</u> maswali.**
xi. **<u>Kunyamaza</u> na kusikiliza kwa makini.(5x1)**



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali yanayofuata

*Mtoto ni kito mzigo mzito*

i) Methali (alama 1)

(b) Kipera hiki kinaendelea kudidimia katika jamii yako.Eleza mbinu tano utakazotumia kukidumisha katika jamii. (al 5)

i. **Kuirithisha fani yenyewe ya utambaji kwa vizazi vya sasa na vijavyo.**
ii. **Kukifanyia utafiti ili kubainisha sifa za uwasilishaji wazo na kuzihifadhi.**
iii. **Kuzihifadhi kwenye maandishi.**
iv. **Kujifunza shuleni.**
v. **Kuzitamba mara kwa mara.**
vi. **Kuzihifadhi kwenye video ili kuhifadhi sifa za uwasilishaji kama vile sauti/kidatu, na miondoko.**
vii. **Kutafitia vyanzo vya kudidimia kwazo ili kuvidhibiti/kuvitatua.**
viii. **Kuandaa mashindano ya kijipera hiki ili kurithisha utambaji wacho kutoka kizazi hadi kingine/kuwafanya vijana wavutiwe nazo.**
ix. **Kufadhili utafiti kuhusu ngano.**
x. **Kushirikisha wageni waalikwa katika ujifunzaji wa kuzifunza kwa mitindo anuwai ili kuwafanya wanafunzi wavutiwe nazo, na kuziendeleza.**
xi. **Kuzitumia kufunzia masomo mengine na stadi nyingine kama vile kusikiliza na kuzungumza.**
xii. **Kuandaa vipindi vya redio au runinga na kuwaalika mafanani stadi kutamba ili kuwa vielelezo.**
xiii. **Kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wake.**
xiv. **Wizara ya elimu kuweka sera zinazohimiza na kulinda utambaji na uhifadhi wa methali.(5x1)**

(c) Kipera hiki kinaenelea kudidimia katika jamii yako.Eleza mbinu tano utakazotumia kukidumisha katika jamii. (al 5)

i. **Fani yenyewe ya utambaji kwa vizazi vya sasa na vijavyo.**
ii. **Kukifanyia utafiti ili kubainisha sifa za uwasilishaji wazo na kuzihifadhi.**
iii. **Kuzihifadhi kwenye maandishi.**
iv. **Kujifunza shuleni.**
v. **Kuzitamba mara kwa mara.**
vi. **Kuzihifadhi kwenye video ili kuhifadhi sifa za uwasilishaji kama vile sauti/kidatu, na miondoko.**
vii. **Kutafitia vyanzo vya kudidimia kwazo ili kuvidhibiti/kuvitatua.**
viii. **Kuandaa mashindano ya utambaji wa ngano ili kurithisha utambaji wazo kutoka kizazi hadi kingine/kuwafanya vijana wavutiwe nazo.**
ix. **Kufadhili utafiti kuhusu ngano.**
x. **Kushirikisha wageni waalikwa katika ujifunzaji wa kipera kuzifunza kwa mitindo anuwai ili kuwafanya wanafunzi wavutiwe nazo, na kuziendeleza.**
xi. **Kuzitumia kufunzia masomo mengine na stadi nyingine kama vile kusikiliza na kuzungumza.**
xii. **Kuandaa vipindi vya redio au runinga na kuwaalika mafanani stadi kutamba ili kuwa vielelezo.**
xv. **Kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wake.**
xvi. **Wizara ya elimu kuweka sera zinazohimiza na kulinda utambaji na uhifadhi wa ngano.(5x1)**



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/
Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

## SEHEMU B :Tamthilia – BEMBEA YA MAISHA - *Timothy* Arege

Jibu swali la 2 au 3.

2. Maisha ya sasa hayana fundi. Yanamwendesha kila mtu kama tawi lililosukumwa hadi likang'oka kutoka taagani na kupeperushwa na upepo….Ulimwengu wa sasa haubagui. Wadogo kwa wakubwa…..

.a) Nukuu

- ✓ Ni **Neema**
- ✓ Kwa **Bela**
- ✓ Wako **nyumbani** kwa akina Neema
- ✓ Ni baada ya Neema kufika kutoka kazini na kumpata Bela jikoni akiosha vyombo, Kuingia kwa Neema **kunamshtua Bela** mpaka mkono inatetemeka **kwa akili zake zilikuwa mbali** **4 x 1 = 4**

**b) Mbinu za Kimtindo**

- ✓ **Jazanda** – Maisha ya sasa hayana fundi – Yaani hayana mwenyewe
- ✓ **Tashbihi** – Yanamwendesha kila mtu kama tawi…
- ✓ **Taswira** – ya tawi liking'oka na kupeperushwa na upepo
- ✓ **Tanakuzi** – wakubwa kwa wadogo
- ✓ **Uhaishaji** – ulimwengu …haubagui 5 x 1 = 5

c) Njia za mtambua msemewa

- ✓ Hayasemayo mhusika- Uzungumzi nafsia wa Neema akimshukuru Mbunju anaonyesha ni mwenye shukrani Mf
- ✓ Matendo ya Mhusika- Neema kumpeleka mamake hospitali inaonyesha mwajibikaji
- ✓ Wasemayo wahusika wengine – Dina kusema kuwa Neema anmejaliwa akili pevu inaonyesha ni mwerevu Mf.
- ✓ Maelezo ya mwandishi au msimulizi -

d) Fafanua mbinu ishi wanazotumia wahusika kukabiliana na hali zao kwa kurejelea bembea ya Maisha (Al 8)

i. **<u>Kutafutiwa matibabu</u>**-Sara anaugua maradhi ya moyo na Neema anamtafutia matibabu bora kukabiliana na hali hii.
ii. **<u>Kuomba msaada</u>**-Sara anaomba msaada kutoka kwa Dina aje kumsaidia mapishi kwa sababu ya ugonjwa wake.
iii. **<u>Kuajiri kijakazi</u>**-Neema inaidi kumuajiri Bela ili kumsaidia malezi kwani yeye na mumewe aghalabu walikuwa kazini.
iv. **<u>Kutafuta mahali pa malazi</u>**-Kwa sababu ya tamaduni Neema anamtafutia Sara malazi kwa Asna kwani Sara hawezi kulala kwa Bunju na Neema.
v. **<u>Kuchukua mkopo kwa benki</u>**-Bunju anamueleza Neema kuwa mkopo aliouchukua kununua nyumba haumpi amani.Mkopo huu unawasaidia kupata nyumba.
vi. **<u>Kujizatiti katika malezi</u>**-Baada ya Yona kufutwa kazi Sara anajizatiti ili kuwalea wanawe Neema,Asna na Salome,



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/
Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

vii. **<u>Kula chakula kidogo</u>**-Kiwa ana changamoto ya kukosa chakula na hivyo basi anajifunga mashombo na kujifunza au kuzoesha tumbo lake kula chakula kidogo.

viii. **<u>Kuambulia ulevi</u>**-Yona baada ya kusemwa na wanajamii kuwa amekosa mtoto wa kiume anaingia katika ulevi kujisahaulisha hali hii.

ix. **<u>Kutafuta kazi</u>**-Asna anaposoma na kukosa kupata kazi anaenda mjini kuishi na kutafuta ajira huko akisema kuwa maisha ni kujaribu

3. Naam, bembea! Hata bembea ikiwa ya kamba au chuma hatimaye hulika. Wanasema papo kwa papo kamba hukata jiwe. Bembea inapolika na kukatika haiwi mwisho wa mchezo. <u>Huungwa na mchezo kuanza tena.</u>

(a) Kuchanganua mtindo katika kifungu. (al 4)

- ✓ **Nidaa**: bembea!
- ✓ **Methali**: papo kamba hukata jiwe
- ✓ **Taswira** muono:Bembea hulika,..hukatika,..huungwa
- ✓ **Jazanda**:Bembea-hali ya maisha

(b) **Toni ya ushauri:**Bembea hukatika na kuungwa tena. Watu wasikate tamaa maishani,

(c) **Kinaya** katika kauli iliyopigiwa mstari.

(i) **Ugonjwa**: Baada ya Sara kupata maradhi na kuwa dhaifu wa mwili Neema anaeleza Yona kuwa Sara ataishi kwa ugonjwa huo milele.

(ii) **Kazi**: Yona alikata bembea yake kikazi baada ya kuzama katika ulevi.Hili lilimfanya apigwe kalamu na kuishi bila kazi hiyo ya ualimu.

(iii) **Watoto-**Licha ya familia ya Yona na Sara kupata watoto Neema,Salome na Asna bado wanajamii wangali nani atakuwa mridhi wa mali ya Yona

(iv) **Elimu:**Licha ya Asna kuwa amesoma na kuhitimu ili aweze` kupata ajira ni kinaya kuwa bado hajafanikiwa kupata kazi kama vile Bunju aneleza Neema.

(v) **Kuajiri wafanyikazi**-: Licha ya Neema kuajiria wazazi wake Yona na Sara wafanyikazi ili waweze kuwasaidia inatokea kuwa kinaya kuwa mmoja anafutwa kwa kukosa uaminifu na mwingine akiacha kaxi kwa kudai kuwa mna kazi nyingi.Bembea hii haijaungika.

(vi) **Tamaduni**-Licha ya Neema kujaribu kuunga bembea ya mtazamo wa Bunju kuhusu tamaduni ya kumruhusu Sara alale kwake Bunju anakataa kuunga Bembea hii huku akidai kuwa mila na tamaduni zina mahali pake. \

(vii) **Malezi**: Licha ya Neema kulalamikia Bela namna malezi hayajawezekana vyema kwake kumlea Lemi kwa sababu ya kazi hana budi kuendelea kufanya kazi lili kukidhi mahitaji ya familia yake

(d) Umuhimu wa mandhari katika Tamthilia

(i) **<u>Hutambulisha wahusika</u>**.mfano nyumbani kwa Yona kunamtambulisha Yona mwenyewe na mke wake Sara.

(ii) **<u>Huonyesha hali ya tukio</u>** k.v migogoro Kwa mfano mgogoro wa Bunju na Neema kuhusu tamaduni unadhihirika nyumbani kwao.

(iii) **<u>Hutambulisha</u> mahali halisi pa tukio** Mfano nyumbani kwa Luka kutambulisha mahali halisi ambako Yona na Beni walihudhuria sherehe.

(iv) **<u>Huibua taharuki</u>**: Mwandishi anatumia mandhari ya nyumba ya Bunju kuleta taharuki kwani hatufahamu alipoondoka ikiwa alipata hela za kuja kumsaidia Neema mke wake.

(v) **<u>Kubainisha maudhui</u>** kama malezi,yanayodhihirika nyumbani mwa Sara na Yona wanapozungumzia kuhusu mwana wao Neema.

(vi) **<u>Hukuza ploti</u>:** Mfano mandhari ya ajali ambako Neema alipata ajali yanaendeleza ploti kwani tunafahamu Neema na Bunju walipatana vipi.

(vii) Hubainisha **<u>sifa za wahusika</u>**.Sifa ya Bunju kuwa **mwenye utu** inadhihirika katika mandhari ya ajali alimwokoa Neema.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

## SEHEMU C: USHAIRI

Jibu swali la 4 au 5

4. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yafuatayo;

Wangu niliyekupenda, leo nitakufukuza
Kuishi umenishinda, waniletea mayaza
Ola vile nimekonda, jasadi nimepooza
Uwache kuniumiza,ni heri mwana kunenda

Ulikuwa wangu nyonda, huba nikaikoleza
Kukupenda kama tunda, embe lenye uliwaza
Ukajigeuza punda, teke umenicharaza
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

Nimekonda kama ngonda, mwandani wanilemaza
Sautiyo ya kinanda, sitaki kusikiliza
Sikutaki bora kwenda, muhibu wanishangaza
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

Mengi ulionitenda, si madogo yakupuza
Nalikupa kila gwanda, uvae na kupendeza
Ulikula na kuwanda, kadiri ulivyoweza
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda.

Kinyume ulipokwenda, nilidhani kuteleza
Na wewe hukujilinda, nyendo mbaya kupunguza
Cha kuvunda kisha vunda, hata ukikifukiza
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

Mja wewe wanishinda, kwa tama wachukiza
Kila kitu unadanda, kingawa cha kuumiza
Huwi ndani ya kibanda, huishi kujitembeza
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

2. a) Nafsi neni – Mpenzi
Wangu niliyekupenda, leo nitakufukuza

Alama 1 kutaja na 1 Kufafanua =2

b) Umuhimu wa kipokeo:
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda 1 x 1 = 1

i) Kimalizio cha ubeti
ii) Msisitizo wa ujumbe wa mashairi
2x1=2

c) Sifa za kiarudhi ubeti 3
i) Mishororo minne



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/
Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

ii) Vipande viwili
iii) Mizani: 8: 8
8: 8
8: 8
8: 8

iv) Vina: nda : za
Nda : za
Nda: za
Za : nda
4x1=4

d) Methali : cha kuvunda hakina ubani (al 4 x 1 = 4)
1x2=2

e) Maudhui ubeti -sita(6)
Kutamauka 2x1=2
Mapenzi

f) Sauti ya mpenzi wake ambayo ni nzuri kama ya kinanda 1x1=1

g) Mshairi anaongea kuhusu mpenzi wake aliyempenda kama embe. Anasema kuwa mpenzi huyo alimgeuka na kukosa shukrani vile punda afanyavyo. Anamsihi mpenzi wake aondoke badala ya kuendelea kumtesa 4x1=4

h) Urudiaji
- ✓ Urudiaji wa silabi – za mf
- ✓ Urudiaji wa mshororo - Kiwagizo
  Uwache kiniumiza , ni heri mwana kunenda 2 x 1 = 2
- ✓ Urudiaji wa neno – nimekonda

5. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Tusizowee kusema, hili ni teuo langu
Huenda huji mapema, -angu huja kuwa tungu
Ikaja kukusakama, na kukuposha kwa Mungu
Pana haja ya kupima.

Neno huwa ni la kwako, likiwa ndani moyoni
Lakini katu si lako, likishavuka menoni
Kwa hivyo likutokako, liweke kwenye mizani
Linaweza kuwa cheko, ama tusi kwa wendani
Pana haja ya kupima.

Vivyo hivyo kwa lebasi, huwa yako kisutuni
Hivyo nina wasiwasi, wambe yako sebuleni
Itavutiya matusi, ya wenzio insani
Wakakuchoma nafusi, kwa mishale ya lisani
Pana haja ya kupima.

Mwana ujuwe ni wako, punje ukiimezele


For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/
Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Lakini katu si wako, nde ukimletele
Akiwa yu ndani yako, ni wa duniya vivile
Ukishishila ni wako, muavye tukakuole
Pana haja ya kupima.

Maisha nayo si yako, utabaradi milele
Ungayaishi ja yako, ni tunu ya maumbile
Mgawa si kufu yako, mshindane hili lile
Akupapo akupako, utaishi pale pale
Pana haja ya kupima.

Ni chetu, chako si chako, ulimwengu huwa vile
Juhudi zingawa zako, wa kufaidi ni wale
Ikifika siku yako, nyono zikukae mbele
Ulichosema ni chako, huwabakiya wawale
Pana haja ya kupima.

Kaseme na moyo wako, ubaini haya yale
Ukuambacho ni chako, kisikupe mageule
Kitu utajacho chako, huenda kiwe cha wale
Na usemacho si chako, kiwe chako ndicho kile
Pana haja ya kupima.

(*Maanga ya Ushairi na Diwani ya Mjileo* - Henry Indindi)

**SEHEMU YA A: USHAIRI**

(a) Pana haja ya kupima 1x1=1
(b) Kuchuja mambo kabla ya utekelezaji 2x1=2
(c)
   i. Mtoto ni wa jamii si wa mzazi tu
   ii. Mavazi katika chumba cha kulala – nje si yako
   iii. Tupime maneno tunayosema

3x1=3

(d)
   i. Takhmisa - mishororo 5 kila ubeti
   ii. Msuko – kibwagizo kina mizani chache/kimefupishwa
   iii. Mathnawi – vipande 2
   iv. Ukaraguni – kila ubeti una mpangilio wa vina vyake (4x1=4)

(e)
Binadamu 1x1=1

(f)
Kutahadharisha/kukanya 1x1=1

(g)
Mshairi anasema kuwa mwana ni wako wakati wa kupata himila. Anasisitiza kuwa mwana si wako akisha kuzaliwa. Hata akiwa tumboni mwako ni wa dunia/jamii. Anaongeza kusema


For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/
Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

kwamba ukishikilia kuwa mwana ni wako jaribu kuavya mimba uonekane. Mshairi anamaliza kwa kusema kuwa ni vyema kuchunguza tunayoyafanya.

4x1=4

(h)

Baadhi ya mifano:

i. Lahaja – Ukishishila (ukishikilia)
- Tukakuole (tukakuone)
- Nde – nje
- Tungu - chungu

ii. Mazida – ukiimezele badala (ukiimeza)
- Ukimletele (ukimleta)

iii. Inkisari – kaseme (sema/ukaseme)
- Vivile (vilevile)
- Ukuambacho – (ukuambiacho)

iv. Kuboronga sarufi – nde ukimletele (ukimletele nde – ukimleta nje)

v. Tabdila – Tuzowele (tulilozoea)
- Duniya (dunia)
- Ujuwe (ujue)
- Tusizowee (tusizoee)
- Huwabakiya (huwabakia)
- Mageule – mageuzi

(Uhuru wowote 3 x1 = 3)

(i)

(i) lebasi - mavazi

(ii) punje ukiimezele – wakati wa kupata himila (2x1=1)

## SEHEMU D : Hadithi Fupi – Mapambazuko ya Machweo

**Mzimu wa kipwerere**

7.“Siku iliyofuata, majira ya magharibi pevu, nilifika pale mzimuni. Kama ilivyo ada yangu, nilivaa guo jeupe lililonifunika gubigubi kama maiti. nikaangalia huku na huko, sikuona mtu. Hapo nikasogea karibu zaidi na ule mzimu. Nilipofika nikauimba ule wimbo wote. Nilipomaliza tu nikajitoma kichakani mle bila hofu wala kimeme…nilichokiona humo, sikuamini macho yangu! Mle ndani ya mzimu mlikuwa na makanda na makasha ya tumbaku, unga wa kilevi na bangi kwenye marobota. Kulikuwa na mapipa ya chang'aa na tembo ya mnazi. Humo pia, mlikuwa na kitanda cha besera kilichotandikwa vizuri. Juu ya kitanda hicho, palitupiwatupiwa asumini na maua ya mlangilangi..”

a)Eleza aina ya taswira katika kifungu hiki.

**Taswira mwendo**- Hapo nikasogea karibu zaidi na …

- ✓ **Taswira oni/muono**-nilichokiona humo, sikuamini macho yangu!/nikaangalia huku na huko
- ✓ **Taswira mnuso**-asumini na maua ya mlangilangi.



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

- ✓ **Taswira sikivu**- nikauimba ule wimbo wote
- ✓ **Taswira hisi**-nikajitoma kichakani mle bila hofu wala kimeme(4x1)

b) Ukirejelea hadithi ya ***" Mzimu wa Kipwerere***," Fafanua jinsi imani katika mambo ya kichawi yamejikita katika jamii. (al 6)

Ni imani potovu kuhusiana na masuala ya ramli, uchawi, mizimu na masuala ya aina hiyo.

i. Inaaminika kwamba Kipwerere alimpata **shetani aliyefichua damu**.Hii ndio maana Kichaka hiki cha kutisha kinachohusiana na matendo yakishetani kikapewa jina Mzimu wa Kipwerere kwani jamaa huyu alizikwa hapa

ii. Pia,haikuruhusiwa mtu **kupita karibu na kichaka hiki cha kutisha majira ya saa sita mchana**.Iwapo kuna mtu atathubutu kupita hapo wakati huo basi atakufa na kutolewa kafara.

iii. Kwa kuongezea, **hakuna mtu aliyeruhusiwa kupita pale majira ya usiku**.Inasemekana kwa wakati huo ndipo mashetani wanaoishi kwenye msitu huo wanafanya shughuli zao. Kwa hivyo, iwapo utavunja miiko hii basi utakufa.

iv. pia, **hakuna mtu aliyeruhusiwa kuingia kwenye msitu** huo kama si mmoja kati ya Wazee wa mji au wale wanaojiita wahenga waliotukuka.Ukithubutu kuingia humo ndani basi utakutana na mashetani watakao kufanya mali yao.

v. Inaaminika kuwa unapopita hapo na usikie watu wakiongea;mume na mke,**basi ujue kwamba shetani pia ana mke** na wako katika harakati zao za kupanga mipango yao.

vi. Pia **kuongea kwa hawa mashetani kwa sauti ya chini** kunaishiria kuwa watoto wao wamelala.Kwa hivyo wanatumia fursa hiyo kushauri anana kupanga mikakati yao ya kuendeleza maisha.

vii. Unapopita karibu na mzimu na usikie harufu kali ya sigara, **basi inaaminika kuwa shetani pia wanavuta sigara.** Kwa hivyo wakati huo wanavuta sigara.Katika kijiji hiki Salihina ndiye akiyeruhusiwa **kufanya kimila kama vile matambiko** iwapo kuna mwanakijiji yeyote amekumbwa na jambo .

viii. Pia iwapo kuna **watoto wanaotaka kupashwa tohara ni lazima waletwe** pale mzimuni ili kuombewa na kupewa baraka na Salihina. Mizimu ikikubali shughuli hiyo ifanyike basi, itafanyika bila madhara yoyote.

ix. Inaaminika kuwa **kukiwa na harusi au sherehe yoyote** kijijini ni lazima Salihina azungumze na mizimu ili hiyo sherehe ifane.

x. Mtu anapotaka **kuingia mzimuni ni lazima awe na ufunguo**. Ufunguo ambao ni wimbo.Ni wale watu wanaojua kuuimba tu ndio wanaoweza kuingia mzimuni. Ilimlazimu msimulizi kujifunza wimbo huu ndipo aweze kuingia kwenye msitu huu.

xi. **Ulaghai kwa sababu ya ushirikina-** Kuna wimbo unaoaminiwa kuwa ufunguo wa kuingia mzimuni. Anausikia kutoka kwa Salihina na kuuimba kisha kuingia. La kushangaza ni kuwa hamwoni shetani yeyote anavyotarajia.Anagundua kuwa Salihina ndiye anaendesha shughuli zote wanazoshuhudia msituni humo.

xii. **Mihadarati kuuzwa huku walanguzi wakitumia woga wa mzimu**-Salihina na Bishoo wanatumia itikadi na imani potovu kuchuuza mihadarati. Bishoo anamweleza mpango wake wa kusafirisha dawa hizo kwa kubeba ndoo wanazodai kuwa wanaenda kuchotea shetani wa mzimu maji. Hata polisi wenyewe wanawaruhusu! Ndoo hizo hatimaye zinajazwa ‘mzigo’; mihadarati.

(6x1)



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

(b)**Mapambazuko ya Machweo –** Clara Momanyi

Onyesha vile **Jua la Macheo** linawabishia wahusika mbalimbali katika **Machweo** yao (al 10)

- ✓ Mapambazuko ya machweo humaanisha kuwa mtu au hali kubadilika na kuwa nzuri wakati wa uzee au kupoteza matumaini na kuwa nzuri.
- ✓ Makucha akiwa bado kijana akifanya kazi (mapambazuko) alistaafishwa bila kutarajia (machweo) hakupewa hata fidia
- ✓ Bi. Macheo mke wa Makucha alikaa pale nyumbani akisubiri siku zake za mwisho duniani-kupoteza matumaini kama jina lake
- ✓ Vijana na Watoto wakiwa bado wachanga (mapambazuko) Maisha yao yaliharibiwa kwa kukosa kwenda shule, na kujiingiza katika mihadarati na kufanyishwa kazi ya kuchimba migodi (machweo) bila elimu kesho yao imefifia.
- ✓ Katika uzee wake mzee Makutwa (machweo) alikuwa anashirikiana na vijana na kustarehe. Anakiri kuwa hata kama ni mzee aliendelea kuishi kama kijana(mapambazuko)
- ✓ Mzee makucha alikuwa amekubali uzee wake kwa majuto mengi, anasema alingoja tu kifo chake. Anaona ujana ulimpita.
- ✓ Mzee makucha anaamini kuwa hata kama amezeeka (machweo) kuna siku atapata afueni (mapambazuko)
- ✓ Sai na Dai ni vijana waliosoma katika chou kiku, wanafanya kazi ya utingo na upagazi.wanaona ingawa ni vijana(mapambazuko) Maisha yao yamegonga mwamba (machweo). Wanaona wamechelwa, tayari wamefika alasiri na hawana kazi.
- ✓ Mzee makutwa alikuwa anaishi Maisha ya kitajiri (mapambazuko) alipofikishwa korokoroni maisha yake ya utajiri yalifikia ukingoni (machweo)
- ✓ Mzee Makucha alikuwa amefika machweo ( amepoteza matumaini) lakini kile kitendo cha kusaidia polisi kumkamata Makutwa kilifanya atunukiwe pesa na tajiri mmoja (mapambazuko)
- ✓ Wale vijana na watoto waliokuwa wamefungiwa pale kwa mgodi kama (machweo) waliokolewa na askari na Makucha. Maisha yao yalipambazuka.



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/